

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAMISEMI



**TAARIFA KWA UMMA**

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2018 wataanza muhula wa kwanza tarehe **16 Julai, 2018**. Wanafunzi wote wanapaswa kuripoti katika Shule aliyopangiwa kwa muda uliopangwa. Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti kwa zaidi ya **siku 14 kuanzia tarehe ya mwisho ya kuripoti**, nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.

Mwanafunzi aliyechanguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, anapaswa **kupakua (Download)** fomu ya kujiunga na shule husika kwenye mtandao. Mwanafunzi hapaswi kwenda kuchukua fomu ya kujiunga katika shule aliyopangwa na haruhusiwi kupiga simu. Aidha, wanafunzi waliopangwa kwenye Vyuo vya Elimu ya Kati inabidi kufanya **UTHIBITISHO** kuanzia tarehe 17 Juni, 2018 hadi ifikapo tarehe 8 Agosti, 2018 wa kukubali kujiunga na **Kozi na Vyuo** walivyopangiwa kwa njia ya mtandao. Uthibitisho huo utafanyika kupitia tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı (NACTE) ya [www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz) katika kiunganishi kinachoitwa **Uthibitisho TAMISEMI**. Mwanafunzi atakayeshindwa kuthibitisha kozi na chuo alichopangiwa, nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine. Mwanafunzi atakayetaka kufanya mabadiliko ya kozi na chuo alichopangiwa ataruhusiwa kufanya hivyo kuanzia tarehe 9 Agosti, 2018 hadi 23 Agosti, 2018 kupitia tovuti ya NACTE ya [www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz).

Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ufundı na Vyuo vya Kati vinavyosimamiwa na NACTE kwa mwaka 2018 pamoja na fomu za kujiunga na shule (joining instructions) inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ya [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı (NACTE) ya [www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz)

**Imetolewa na Katibu Mkuu,  
OR-TAMISEMI**